# KANUNI ZA UTENDAJI WA WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU WAKATI WA UCHAGUZI NA MICHAKATO YA KIDEMOKRASIA NCHINI TANZANIA



(Zimetungwa chini ya Ibara ya 6 na 37 ya Katiba ya Mtandao na aya ya 7.1 ya Sera ya Wanachama wa Mtandao)

OKTOBA 2019

## MHARIRI

- Onesmo Olengurumwa

Mratibu kitaifa- THRDC

## WAANDISHI

- Wakili Joyce Eliezer
- Wakili Leopold Mosha
- Wakili Deogratias Bwire
- Paul Kisabo

## MSANIFU

- Deogratius Chambi

  Mtaalamu wa Teknolojia na Digitali-THRDC

## MSAMBAZAJI

- Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania

## MAWASILIANO


+255 769 642 208

info@thrdc.or.tz

www.thrdc.or.tz


©THRDC 2019

# YALIYOMO


**VIFUPISHO** . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . i

**UTANGULIZI** . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . ii

**SHUKRANI** . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . v

**TAFSIRI** . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . vi

**MUHTASARI** . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . viii

**DIBAJI** . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1

- 1.0 Utangulizi . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1
- 1.1 Kanda za Uratibu za Mtandao . . . . . . . . . . 2
- 1.2 Makundi 9 ya Haki za Binadamu . . . . . . . . . 3
- 1.3 Umuhimu wa Kanuni za Utendaji wa Watetezi . . . 3
- 1.4 Demokrasia . . . . . . . . . . . . . . . . . . 4
- 1.5 Nguzo Kuu za Demokrasia . . . . . . . . . . . . 5
- 1.6 Uchaguzi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 6
- 1.7 Kazi za Watetezi wa Haki za Binadamu Kipindi cha Uchaguzi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 7
- 1.8 Watetezi wa Haki za Binadamu . . . . . . . . . 7
- 1.9 Haki za Watetezi wa Haki za Binadamu Nyakati za Uchaguzi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 8
- 1.10 Tamaduni na Misingi ya Watetezi wa Haki za Binadamu . . . . . . . . . . . . . . . . . . 16

**KANUNI ZA UTENDAJI** . . . . . . . . . . . . . . . 19

- 2.0 Malengo ya Kanuni . . . . . . . . . . . . . . 19
- 2.1 Wigo wa Kanuni . . . . . . . . . . . . . . . . 20

**UTEKELEZAJI NA USIMAMIZI WA KANUNI** . . . . . . . . 23

- 3.0 Utekelezaji . . . . . . . . . . . . . . . . . 23

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AZAKI | Asasi Za Kiraia |
| HRC | Kamati ya Haki za Binadamu |
| HRDs | Wtetezi wa Haki za Binadamu |
| ICCPR | Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa |
| NEC | Tume ya Taifa ya Uchaguzi |
| NGOs | Mashirika Yasiyo ya Kiserikali |
| OHCHR | Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu |
| THRDC | Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania |
| ZCU | Kiongozi wa Kanda |
| ZEC | Tume ya Uchaguzi Zanzibar |

# UTANGULIZI

Sisi Wanachama wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC)/Watetezi wa Haki za Binadamu (HRDs);

**Kwa Kuhamasishwa** na misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977), hasa Ibara ya 8 (1), ambayo inasisitiza kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi ambayo inafuata Kanuni za kidemokrasia na haki za kijamii. Na wananchi ndio msingi wa mamlaka yote, na Serikali hupata madaraka na mamlaka yake kutoka kwa wananchi.

**Kwa Msisitizo**, Ibara ya 8 (1) (d) ya katiba, inaeleza kwamba wananchi watashiriki katika shughuli za Serikali yao kwa mujibu wa masharti ya Katiba

**Kwa Kuzingatia**, Mkataba wa Afrika juu ya Demokrasia, Uchaguzi na Utawala 2007, unalenga katika kuendeleza, uzingatiaji, wa kila taifa kwa maadili na kanuni za demokrasia na kuheshimu haki za binadamu katika uchaguzi na michakato mingine ya kidemokrasia.

**Kuthibitisha** Umoja wetu kwa kufanya kazi kwa pamoja bila kuchoka, kupanua na kuimarisha utawala wa sheria, amani, usalama na maendeleo katika nchi yetu kwa kushiriki kikamilifu katika uchaguzi na michakato ya Kidemokrasia;

**Kuongozwa** na dhamira yetu ya kuimarisha taasisi kwa uongozi bora, umoja na mshikamano katika nchi yetu wakati wa uchaguzi na michakato wa kidemokrasia;

**kujidhatiti** kukuza maadili na kanuni zote za kidemokrasia, utawala bora, haki za binadamu na maendeleo;

**kukumbuka** kazi ya watetezi wa haki za binadamu wakati wa uchaguzi na kusisitiza masuala ya kutopendelea upande wowote, uwajibikaji, kutokushiriki moja kwa moja kwenye siasa, uadilifu na kutokuegemea upande wowote wakati wa uchaguzi;

**kuhusu** changamoto za ndani na nje zinazowakabili watetezi wa haki za binadamu (HRDs) Tanzania, ambazo zinazuia utekelezaji wa kazi zao wakati wa uchaguzi na michakato ya kidemokrasia kwa kiwango cha juu:

**kuzingatia** ukweli kwamba watetezi wa haki za binadamu wamekuwa na majukumu makubwa katika kipindi cha uchaguzi, kuanzia utoaji wa elimu ya uraia, wapiga kura, uangalizi wa uchaguzi, na shughuli nyingine kabla ya uchaguzi, wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi.

**Kiu** ya kuondoa dhana potofu kuwa watetezi wa haki za binadamu wamekuwa wakijihusisha na shughuli za kisiasa moja kwa moja hasa kipindi chauchaguzi

**Hivyo basi**, Sisi Wanachama wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania / HRD, tumekubaliana kama ifuatavyo:

**Zimepitishwa na Bodi ya Wakurugenzi (THRDC) Oktoba 2019 na kuidhinishwa na Wanachama wa Mtandao Novemba 16, 2019**

# SHUKRANI

Utayarishaji wa kanuni hizi umefanikiwa kwa sababu ya juhudi na ushirikiano wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania, wanachama wa THRDC, watetezi wa Haki za Binadamu na wadau wa maendeleo. Tunapenda kutambua michango yao mikubwa katika kipindi chote cha uandishi wa kanuni hizi.

Maneno ya shukrani zaidi yawafikie wadau wa maendeleo. Pongezi za dhati zielekezwe kwa Mratibu wa Kitaifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania, Bwana Onesmo Paul Olengurumwa kwa mwongozo wake kuanzia hatua ya awali hadi kufikia tamati.

Mwongozo wake wa kitaaluma, maoni na ukosoaji wake umewezesha kukamilika uandishi wa kanuni hizi. Pongezi za dhati zielekezwe kwa Sekretarieti ya THRDC, wakili Joyce Eliezer, Bwana Paul Kisabo, Wakili Leopold Mosha na Wakili Deogratias Bwire kwa ustadi wao na juhudi zao bila kuchoka katika kuandika kanuni hizi.

Shukurani za kipekee ziende kwa wahariri kwa msaada wao katika kusoma, kuhariri na kutoa maoni yao juu ya yaliyomo hadi kuwa na rasimu ya kanuni hizi

# TAFSIRI

**Shughuli za kisiasa**- itajumuisha shughuli za vyama vya siasa au shughuli zinazohusiana na vyama vya siasa kama vile kugombea nafasi za kisiasa, kampeni za kisiasa, kujihusisha na shughuli za kutafuta fedha kwa ajili ya siasa za vyama, kutumika kama mdhamini wa chama cha siasa, kuwa na uongozi ndani ya ofisi ya chama cha siasa, kuvaa nguo kichama, beji au itikadi, kukubali upendeleo kutoka kwa vyama vya siasa au wagombea, kuwa mwakilishi wa chama cha siasa.

**Elimu ya Uraia** – maana yake ni kutoa elimu, uzoefu wa kujifunza ili kuwezesha na kuwawezesha wananchi kushiriki katika michakato ya kidemokrasia.

**Kanuni za Utendaji wa HRDs-** maana yake ni mjumuiko wa kanuni, maadili, mwongozo, sheria, makatazo na majukumu au vitendo sahihi vya, HRDs au mwanachama wa Mtandao nyakati za uchaguzi na michakato ya kidemokrasia.

**Shughuli za Kawaida za Uchaguzi** -hizi ni pamoja na shughuli zote zinazokubalika kiulimwengu na kufanywa na watetezi wa haki za binadamu nyakati za uchaguzi: nazo ni pamoja na utoaji wa elimu ya uraia, mpiga kura, ufuatiliaji na uangalizi wa uchaguzi, kutoa ilani za uchaguzi kwa umma, kutetea mabadiliko ya sheria za uchaguzi, kutetea uchaguzi huru na wa haki, kukosoa dosari zilizojitokeza katika ucha-

guzi, kuhimiza amani na usalama wakati wa uchaguzi.

**Nyakati za Uchaguzi-**inajumuisha nyakati tatu za uchaguzi: kabla ya uchaguzi, wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi.

**Mtetezi wa Haki za Binadamu** – maana yake ni mtu yeyote au shirika linalotetea haki za binadamu kutoka makundi mbalimbali ya haki za binadamu kama ilivyoainishwa katika kanuni hizi.

**Kutofungamana na Chama-** maana yake ni kutopendelea itikadi za kisiasa, haswa kuelekea kundi fulani la kisiasa au mgombea.

**Kutoegemea Upande wa Kisiasa –** Maana yake ni kutoegemea upande wowote, kufanya kazi kwa uhuru, usawa, kuzingatia haki, uwiano na uwazi wa mawazo.

**Kiongozi wa Kanda-** maana yake ni Shirika lililoteuliwa na Mratibu wa Kitaifa wa THRDC kwa mujibu wa Miongozo ya Utendaji Kazi za viongozi wa Kanda (ZCUs)

# MUHTASARI

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania ni shirika lisilo la kiserikali lenye wanachama binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali 200, Tanzania Bara na Zanzibar. Wanachama wake wote ni watetezi wa haki za binadamu.

Wanachama wa THRDC na HRDs kwa muda mrefu wamekuwa wakijihusisha na shughuli mbalimbali nyakati za uchaguzi na michakato ya kidemokrasia bila kuwa na sera, sheria au kanuni za utendaji kazi za kuwaongoza. Hii imesababisha uwepo wa malalamiko dhidi ya HRDs kuwa wanajihusisha moja kwa moja kwenye shughuli za kisiasa.

Ili kutibu kasoro hiyo, THRDC imeandaa kanuni hizi ili kuwaongoza wanachama na HRDs wanaofanya shughuli mbalimbali nyakati za uchaguzi na michakato ya kidemokrasia. Kanuni hizi zimetoa miongozo ambazo HRDs lazima wazingatie ili kuhakikisha ushiriki na ufanisi wa utendaji kazi katika nyakati za uchaguzi na michakato ya Kidemokrasia nchini. Kanuni hizi zina sehemu tatu.

**Sehemu ya Kwanza inaelezea utangulizi,** maana ya demokrasia, nguzo kuu za demokrasia, uchaguzi, maana ya Watetezi wa Haki za Binadamu na haki zao, maadili na kanuni za msingi ambazo HRDs wanapaswa kuzingatia.

**Sehemu ya Pili ni ya msingi zaidi,** sababu inajumuisha kanuni ambazo wanachama wa THRDC na watetezi wa haki za binadamu lazima kuzingatia nyakati za uchaguzi na michakato ya kidemokrasia nchini Tanzania.

**Sehemu ya Tatu kimsingi inaelezea mfumo wa utekelezaji** wa kanuni za utendaji za HRDs. inasema kwamba, utekelezaji wa kanuni hizi utasimamiwa kwa mujibu wa Katiba ya THRDC.

# DIBAJI

## 1.0 Utangulizi

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania ni shirika lisilo la kiserikali lenye wanachama binafsi na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali 200. Wanachama wake wote ni watetezi wa haki za binadamu. Dhumuni kuu la Mtandao ni kuhakikisha kwamba kuna mazingira salama, mazuri na endelevu kwa watetezi wa haki za Binadamu nchini Tanzania. Pia kuwatetea na kuwalinda watetezi wa haki za binadamu nchini ikiwemo kuhakikisha kwamba watetezi wa haki za binadamu wanaendelea kuwa katika mazingira salama.

Wanachama wa Mtandao wapo katika kila Mkoa Tanzania bara na Zanzibar, kwa ujumla wamegawanyika katika Kanda 11. Kila Kanda huongozwa na Mratibu wa Kanda (ZCU). Lengo ni kukuza ushiriki wa wanachama kuanzia ngazi ya chini.

## 1.1 Kanda za Uratibu za Mtandao

| NA | KANDA | MIKOA |
|---|---|---|
| 01 | Kanda ya Mashariki na Pwani | Dar es Salaam Pwani |
| 02 | Kanda ya Kati | Dodoma, Morogoro na Singida |
| 03 | Kanda ya Ziwa | Mwanza, Mara na Simiyu |
| 04 | Kanda ya Kaskazini | Kilimanjaro, Arusha, Tanga na Manyara |
| 05 | Kanda ya Kusini | Iringa na Njombe |
| 06 | Kanda ya Nyanda za juu Kusini | Mbeya, Songwe na Rukwa |
| 07 | Kanda ya Kusini Mashariki | Ruvuma, Mtwara na Lindi |
| 08 | Kanda ya Magharibi | Tabora, Kigoma na Katavi |
| 09 | Kanda ya Ziwa Magharibi | Kagera, Geita na Shinyanga |
| 10 | Kanda ya Pemba | Mkoa wa Kusini na Kaskazini Pemba |
| 11 | Kanda ya Unguja | Mkoa wa Kusini, Kaskazini na Mjini Magharibi |

Kwa sasa katika hizo kanda 11, Mtandao una mashirika wanachama 183 na wanachama binafsi 17. Wanachama wote hawa hujihusisha katika shughuli mbalimbali kwenye jamii. Na wamejikita zaidi katika kukuza na kulinda haki za binadamu nchini Tanzania.

## 1.2 Makundi 9 ya Haki za Binadamu

Wanachama wa Mtandao wamegawanyika katika makundi 9 ya haki za Binadamu, kama ifuatavyo:




Wakati wa utekelezaji wa mpango mkakati wa kwanza wa Mtandao mwaka (2012 – 2018). Mtandao kupitia mpango mkakati huo ulilenga zaidi katika kuimarisha taasisi, kujijengea uwezo wa kulinda na kutetea watetezi wa haki za binadamu.

## 1.3 Umuhimu wa Kanuni za Utendaji wa Watetezi

Kwa kipindi kirefu, wanachama wa Mtandao pamoja na watetezi wa haki za binadamu wamekuwa wakishiriki

kwenye nyakati za uchaguzi na michakato ya kidemokrasia bila kuwa na sera, sheria au kanuni za kuzingatia wakati wa utendaji wa kazi hizo. Hii imepelekea kuwepo kwa malalamiko dhidi ya wanachama na watetezi wa haki za binadamu kuwa wamekuwa wakijihusisha na siasa moja kwa moja.

Lakini pia, wakati wa chaguzi zilizopita, watetezi wa haki za binadamu wamekuwa wakikumbana na vitisho mbalimbali vya kiusalama kama vile, kutekwa, kukamatwa na vitisho mbalimbali vya namna hiyo.

Ili kutatua changamoto hizo, Mtandao umeona umuhimu wa kutengeneza kanuni za utendaji kazi wa watetezi wa haki za binadamu kwenye nyakati za uchaguzi na michakato ya kidemokrasia. Kanuni hizi zitakuwa ni mwongozo rasmi kwa wanachama na watetezi wa Haki za Binadamu kwenye nyakati za uchaguzi na michakato yote ya kidemokrasia watakayoshiriki.

## 1.4 Demokrasia

Kwa mujibu wa Rais wa 16 wa Marekani, Ndg. Abraham Lincoln, demokrasia ni serikali ya watu, iliyochaguliwa na watu, na hufanya kazi kwa ajili ya watu. Demokrasia ni mfumo wa Serikali ambayo raia wote wako sawa mbele ya sheria na wanahusika katika kufanya maamuzi moja kwa moja au kupitia kwa viongozi waliochaguliwa. Ni utawala wa watu, na watawala hutawala kwa ridhaa ya watu.

Kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977, Tanzania ni Nchi ya kidemokrasia yenye mamlaka yanayotokana na watu. Kifungu cha (8) cha katiba kinasema, "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi ambayo inafuata Kanuni za kidemokrasia na haki za kijamii," kwasababu hiyo watu ndio wenye mamlaka yote, na serikali itakuwa na nguvu pamoja na mamlaka kutoka kwa watu kwa mujibu wa katiba. Serikali itawajibika kwa watu.

Ibara ya 4 ya Mkataba wa Afrika juu ya Haki za Demokrasia, Uchaguzi na Utawala inahimiza nchi wanachama kujitolea katika kukuza demokrasia, utawala wa sheria na kuzingatia haki za binadamu. Inasisitiza zaidi kwamba, nchi wanachama lazima zitambue ushiriki wa wananchi kwa wigo mpana katika masuala yote ya haki za binadamu.

## 1.5 Nguzo Kuu za Demokrasia

Dhana ya demokrasia ina nguzo kuu tano, ambazo ni; Ukweli na uwazi, uchaguzi huru na wa haki, utawala bora, mgawanyo wa mamlaka na usawa mbele ya sheria. Nguzo hizi za demokrasia zinahakikisha haki na uhuru wa watu na ni muhimu kwa jamii yenye ufanisi wa kidemokrasia ambapo raia wote ni sawa. Ni ndoto ya Watetezi wa Haki za Binadamu kuiona Tanzania inazingatia kanuni za kidemokrasia.

Hivyo basi, demokrasia ni mfumo wa Serikali ambayo mamlaka na uwajibikaji wake husimamiwa na raia wote moja

kwa moja, au kupitia wawakilishi wao waliowachaguliwa kwa uhuru. Demokrasia hutegemea kanuni za utawala wa wengi na uzingatiwaji wa haki za raia

## 1.6 Uchaguzi

Uchaguzi ni mchakato rasmi unaofanywa na kundi la watu ambao huchagua mtu wa kuwaongoza. Kupitia mchakato huu; raia wanahusika katika kuchagua watu ambao watakuwa ni viongozi wa nchi yao. Ili kuhakikisha ushiriki wa umma katika uchaguzi, HRDs na makundi mengine ndani ya jamii yatafanya kampeni za kutoa hamasa, elimu ya uraia na kupiga kura na mambo mengine muhimu yanayo shabihiana.

Ibara ya 2 (13) ya Mkataba wa Afrika juu ya Demokrasia, Uchaguzi na Utawala inahimiza kuendeleza shughuli bora katika mchakato mzima wa usimamizi wa uchaguzi kwa madhumuni ya utulivu wa kisiasa.

## 1.7 Kazi za Watetezi wa Haki za Binadamu Kipindi cha Uchaguzi

| Kabla ya uchaguzi | Siku ya uchaguzi | Baada ya ucha-guzi |
|---|---|---|
| i) Uangalizi wa usajili wa wapiga kura<br>ii) Kutoa elimu ya uraia na ya mpiga kura<br>iii) Kushiriki kwenye mchakato wa mabadiliko ya kikatiba na kisheria<br>iv) Uangalizi wa uteuzi wa wagombea wa vyama vya siasa<br>v) Uangalizi wa kampeni za uchaguzi<br>vi) Kuandaa ilani za uch-aguzi | i) Kufanya ukaguzi kwenye vituo vya kupigia kura<br>ii) Kufanya uangalizi wa upigaji kura na zoezi zima la kuhesa-bu kura<br>iii) Kufanya uangalizi wa utangazaji wa matokeo ya ucha-guzi | i) Kutatua migogoro Vikao vya kufanya tathmini ya ucha-guzi<br>ii) Kutoa ripoti za uangalizi wa uch-aguzi |

## 1.8 Watetezi wa Haki za Binadamu

Watetezi wa Haki za Binadamu ni watu ambao, kibinafsi au kwa pamoja, wanakuza na Kulinda haki za Binadamu. Watetezi wa Haki za Binadamu wana tambulika popote kwa matendo yao, kwa mantiki hiyo wanaelezeka kwa matendo yao sambamba na shughuli wanazo zifanya.

Kazi za Watetezi wa Haki za Binadamu zinatambulika kisheria na zinakubalika kwenye jamii wanazoziwakilisha.

Kila siku, Duniani mamia ya Watetezi wa Haki za Binadamu hukumbana na changamoto za kisiasa kutokana na shughuli

zao za utetezi wa haki za watu wengine. Hii imepelekea kuhatarisha usalama wa maisha yao, wakati wakiijitahidi kutokomeza ukiukwaji wa haki za binadamu na kuendeleza haki za kijamii na kudumisha amani.

Mwaka 1998 Baraza Kuu la umoja wa Mataifa, lilipitisha "Azimio la Haki na Wajibu wa Watu Binafsi, Makundi na Vyombo vya Jamii Kuendeleza na Kulinda Haki za Binadamu zinazotambulika katika misingi ya uhuru.

Kwa lugha nyingine, miaka hamsini baada ya Azimio la Ulimwengu juu Haki za Binadamu, na baada ya miaka ishirini ya mazungumzo ya tamko la rasimu juu ya watetezi wa haki za binadamu, Umoja wa Mataifa hatimae ulitambua yaliyo ya kweli: kwamba maelfu ya watu wamekuza na kuchangia ulindwaji wa haki za binadamu duniani kote. Hili ni Azimio ambalo limeheshimu kwa kiasi watu wanaohusika katika kuendeleza na kulinda haki za binadamu.

## 1.9 Haki za Watetezi wa Haki za Binadamu Nyakati za Uchaguzi

### i) Haki ya kupiga au kupigiwa kura

Ibara ya 21(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,1977 ina eleza kwamba,

"…kila raia wa Jamhuri ya Muungano anayo haki ya kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi, ama moja kwa moja au

kwa kupitia wawakilishi waliochaguliwa na wananchi kwa hiari yao, kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na sheria au kwa mujibu wa sheria".

Ibara ndogo ya (2) ya Ibara hiyo ya Katiba inaeleza kuwa, kila raia (HRDs pamoja) ana haki na uhuru wa kushiriki kwa ukamilifu katika mchakato wa kufanya maamuzi juu ya masuala yanayoathiri wananchi na ustawi wa taifa.

Kwa hiyo, haki ya kupiga kura na / au kwa kupigiwa kura ni msingi katika taifa lolote la kidemokrasia na kama hii haki ya msingi ikikiukwa au kubatilishwa, demokrasia katika maana yake ya msingi itaondoshwa.

### ii) Haki ya kushiriki katika masuala ya umma na uchaguzi

Hii inamaana ya kwamba wananchi wanayo haki ya kushiriki au kugombea nafasi kwenye ofisi za umma, kupiga kura wakati wa uchaguzi na kupata kwenye ofisi za umma. Kikanuni uchaguzi unapaswa kuwa wa huru na wa haki kwenye nchi ya kidemokrasia. Watetezi wa Haki za Binadamu wana haki ya kutetea usawa wa watu wote kupata nafasi kwenye ofisi za umma kwenye shughuli za uchaguzi.

Watetezi wa Haki za Binadamu wanatakiwa kuhakikisha kuwa makundi yote ya watu katika nchi yana fursa sawa katika kupata huduma za umma na maslahi yao yanapaswa

kuzingatiwa. Mfano mzuri ni kwamba, kila mara uchaguzi ufikapo, Asasi Za Kiraia huandaa ilani ya uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu. AZAKI hupendekeza mambo ya kuzingatiwa na wagombea wa kisiasa na serikali ikiwa ni mahitaji ya watu kwa wakati husika.

Mfano, kwa mwaka wa uchaguzi wa 2019/2020, AZAKI zimeainisha vipaumbele kumi (10) ikiwa ni pamoja na kuzingatia usawa wa kijinsia na kuheshimu haki za makundi maalum.

Katika nyakati za kushiriki kwenye shughuli za umma na kwenye uchaguzi wanachama wa (THRDC) na HRDs wana haki ya kutoa elimu ya uraia na kupiga kura baada ya kupata vibali kutoka kwenye mamlaka zinazohusika na uchaguzi. Watetezi wa Haki za Binadamu wanapaswa kuitumia haki hii kwa ufanisi kwenye nyakati zote za uchaguzi.

### iii) Haki ya kulindwa

Utambuzi wa kisheria na ulinzi wa watetezi wa haki za binadamu ni muhimu ili kuhakikisha kuwa wanaweza kufanya kazi katika mikono salama, kudumisha mazingira, bila ya mashambulizi, ghasia na vikwazo vya kisheria visivyo vya ulazima. Azimio la Umoja wa Mataifa juu ya watetezi wa Haki za Binadamu, linatoa wajibu wa kulindwa kwa Watetezi wa Haki za Binadamu katika Nchi wanachama. Ibara ya 2, 9 and12 ya Azimio la Umoja wa Mataifa, zinaeleza kwamba,

Nchi wanachama zinajukumu la kuwalinda HRDs, chini ya mamlaka yao, bila kujali hali zao au misimamo yao ya kiitikadi.

Zaidi ya hayo, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa ambao una nguvu kisheria, chini ya ibara ya 2 unatoa wajibu kwa mataifa kuhakikisha haki sawa kwa watu wote bila kuwabagua.

### iv) Haki ya kushiriki katika kufanya maamuzi

Hii ni haki ya msingi katika taifa lolote la kidemokrasia, Watetezi wa Haki za Binadamu wana haki ya kushiriki katika kufanya maamuzi na kutoa maoni yao au maoni kwa maslahi ya watu katika Taifa bila vikwazo vyovyote vya manyanyaso au kiubaguzi. Umma unapaswa kushiriki katika maamuzi yanayohusu maslahi ya Taifa ambayo yanaweza kuwa ya kisiasa, kijamii, kiuchumi, au kiutamaduni.

Ni muhimu kuzingatia "ushiriki" ikimaanisha "mapenzi ya watu katika kufanya maamuzi, kukubalika kwa maamuzi, uhalali wa kisiasa kuhusu mahitaji na vipaumbele vya watu binafsi, jamii na makundi mbalimbali". Hii haiwezi kupuuzwa kwa Watetezi wa Haki za Binadamu, kama wakihitaji kutoa maoni yao juu ya maendeleo ya demokrasia ya taifa ikiwa ni pamoja na kushiriki katika uchaguzi na michakato wa kidemokrasia.

### v) Haki ya uhuru wa kujumuika na kufanya mikutano kwa amani

Uhuru wa kujumuika, ni pale ambapo mtu huamua kujumuika na wengine bila kubuguziwa pasipo sababu za msingi. Uhuru wa kukusanyika ni uhuru wa kukutana na wengine kwa kusudi au malengo maalumu. Kwa hiyo, Watetezi wa Haki za Binadamu wana haki ya kukutana pamoja na watu wengine kwa ajila ya kuhamasisha, kukuza, kuendeleza na / au kutetea maslahi ya pamoja.

Ibara ya 20 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa haki ya uhuru wa kujumuika na wengine. Zaidi ya hayo, kati ya malengo ya Sera ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001, ilikuwa kuweka taratibu za usajili ambazo ni za wazi kwa mashirika yasiyo ya kiserikali, madaraka na ambayo yanawezesha kuratibu ubora wa mashirika yasiyo ya kiserikali wakati wa kulinda uhuru wa kujumuika.

Hii haki pia inatambuliwa na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR), Mkataba wa Afrika juu ya Haki za Binadamu na Watu (ACHPR), na Mkataba wa Afrika wa Demokrasia Uchaguzi na Utawala, miongoni mwa mikataba mingine ya haki za binadamu. Watetezi wa Haki za binadamu wana uhuru wa kujumuika na kufanya mikutano ya amani kwa ajili ya kutetea masuala mbalimbali juu ya uwajibikaji na haki za HRDs na wananchi wengine.

Haki ya uhuru wa kujumuika inatoa hakikisho la uhuru kwa watetezi wa Haki za Binadamu kujiunga uanachama katika chama cha siasa kwa hiari au ridhaa yao wenyewe. Kwa hiari yake binasi, Mtetezi wa Haki za Binadamu ana haki ya kumpigia kura kiongozi katika hicho chama cha siasa. Kinacho zuiliwa ni ushiriki wa moja kwa moja katika shughuli za chama hicho cha siasa

### vi) Haki ya kukosoa kwa lengo la kujenga

Katika nchi za kidemokrasia, wananchi ndio msingi wa mamlaka yote. Wananchi hukabidhi baadhi ya haki zao kwa viongozi wa serikali kwa ajili ya ulinzi. Aina hii ya uhusiano inajulikana kama mkataba wa kijamii au kisiasa kati ya wananchi na serikali.

Mkataba huu wa kijamii au kisiasa ni makubaliano kati ya wananchi na serikali. Wananchi hukubali kufuata sheria zilizotungwa na kusimamiwa na serikali. Sheria hizo zipo kwa ajili ya kuhakikisha kuwa haki za wananchi zinalindwa. Haki zisipolindwa wananchi wana haki ya kuikosoa serikali.

Kwa hiyo, kuikosoa serikali sio tu ni haki, lakini pia ni wajibu wa kila raia na Watetezi wote wa Haki za Binadamu. Ukosoaji ni msingi wa kuziwajibisha mamlaka zilizowekwa na wananchi juu ya majukumu yao. Hivyo basi kama raia yeyote anavyo paswa kuwajibika, watetezi wa haki za binadamu pia wana wajibu wa kuiwajibisha serikali kwa kuikosoa, ku-

toa mapendekezo juu ya nini kifanyike. Watetezi wa haki za Binadamu wanaweza kushirikiana na vyombo vya serikali moja kwa moja katika mijadala juu ya kupitishwa kwa mapendekezo yao na kufuatilia kwa ukaribu utekelezaji wake.

### vii) Haki ya maandamano ya amani

Haki ya kuandamana ni haki ya binadamu ambayo inatambuliwa na mikataba mbalimbali ya haki za binadamu. Wakati hakuna mkataba wa haki za binadamu au katiba inayotoa moja kwa moja haki ya kuandamana, haki hiyo ya kuandamana inaweza kudhihirishwa kwenye haki ya uhuru wa kukutana, haki ya uhuru wa kujumuika, na haki ya uhuru wa kujieleza.

Ina maana ya watu kujumuika kwa wakati fulani na kueleza malengo yao juu ya jambo fulani. Kuandamana, hata hivyo, sio lazima pawe na vurugu au tishio juu ya maslahi ya usalama wa taifa au usalama wa wananchi. Wala sio lazima pawe na ukiukwaji wa sheria, sababu maandamano si lazima kuhusisha ukiukwaji wa sheria za nchi.

### viii) Haki ya uhuru wa maoni na kujieleza

Hii haki inamaanisha, uhuru wa kutoa maoni bila kuingiliwa, haki ya kupata taarifa na kutoa habari na kila aina ya maoni kupitia Vyombo vya Habari bila kujali mipaka, iwe ni kwa mdomo, maandishi au kuchapisha, katika muundo wa sa-

naa, au kwa njia nyingine yoyote. Kimsingi uhuru wa kujieleza ni pamoja na uhuru wa Vyombo vya Habari.

Haki ya uhuru wa kujieleza inajumuisha pia matumizi ya mitandao na kutoa maoni au kujieleza. Huu uhuru ni muhimu kwa wananchi kuiwajibisha Serikali, mashirika na maafisa, kwa kuonyesha wasiwasi wao na maoni kupitia majukwaa na vyombo vya habari vyenye kuwapendeza.

Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 inalinda uhuru wa kujieleza. Ni moja ya haki za ushiriki - haki muhimu kwa wananchi kushiriki kutoa maoni kuhusu utawala. Kwa mujibu wa Kamati ya Haki za Binadamu (HRC), haki hii 'ni haki ya muhimu kwaajili ya utekelezaji wa kanuni za uwazi na uwajibikaji katika nchi za kidemokrasia, Pia ni ya muhimu kwaajili ya kukuza na kulinda haki za binadamu katika uchaguzi na michakato wa kidemokrasia.

### ix) Haki ya kutafuta rasilimali

Wanachama wa THRDC na Watetezi wa Haki za Binadamu wana haki ya kuomba au kutafuta rasilimali kwa lengo la kushiriki katika shughuli mbalimbali za uchaguzi na michakato ya kidemokrasia. Rasilimali hizo ni kwaajili ya shughuli kama vile: kutoa elimu ya uraia na upigaji kura, mijadala ya umma, kuandaa ilani au ajenda za uchaguzi na kidemokrasia au ilani na kufanya uangalizi wa uchaguzi.

## 1.10 Tamaduni na Misingi ya Watetezi wa Haki za Binadamu

Wakati wa kutekeleza hizi kanuni, HRDs watahitajika kukuza na kulinda tamaduni na misingi ifuatayo:

**a)** Watetezi wa haki za Binadamu katika nyakati za uchaguzi, hawapaswi kujihusisha moja kwa moja na chama cha siasa, mgombea wa cheo cha kisiasa, mwanasiasa (Kanuni ya Kutofungamana na Chama)

**b)**Watetezi wa Haki za Binadamu wanapaswa kuwa na matumizi sahihi ya rasilimali walizopewa na wafadhili, na wanapaswa kuhakikisha kwamba wanazitumia kwa madhumuni yaliyokusudiwa (Kanuni ya Utunzaji)

**c)**Watetezi wa haki za Binadamu ni lazima waeleze ni kwa jinsi gani wametumia rasilimali zao na matokeo waliyoyapata, kwa wadau wote, ikiwa ni pamoja na walengwa (Kanuni ya Uwajibikaji)

**d)**Watetezi wa Haki za Binadamu wanapaswa kufanya kazi zao kwa uwazi, kutoa taarifa za shughuli zao na mipango yao kwa wadau (kanuni ya Uwazi).

**e)**Watetezi wa Haki za Binadamu wanapaswa kufanya kazi kwa uadilifu na kwa ufasaha nyakati za uchaguzi (kanuni ya Uadilifu)

**f)**Wanachama wa THRDC pamoja na Watetezi wa Haki za Binadamu, wanaoshiriki shughuli mbalimbali nyakati za uchaguzi na kwenye michakato ya kidemokrasia, watakongozwa na kanuni hizi bila kupendelea upande wowote na bila kumbagua mgombea yeyote.

**g)**Mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu za fedha na nyaraka wakati wa uchaguzi, HRDs wanapaswa kuzingatia viwango vya uhasibu vya kimataifa.

**h)**Vikwazo vyovyote wakati wa uchaguzi ambavyo vinaweza kuwekwa dhidi ya Watetezi wa Haki za Binadamu kuhusiana na uhuru wa kujieleza, maandamano ya amani na kujumuika lazima vizingatie viwango vya kisheria vya kimataifa.

**i)**Watetezi wa Haki za Binadamu wanapaswa kufanya kazi zao kwa amani na katika mazingira ya ukarimu, bila hofu ya kunyanyaswa, kulipiziwa kisasi, vitisho na ubaguzi nyakati za uchaguzi.

**j)**Kutambua mamlaka za serikali katika kusimamia mashirika ndani ya nchi kwa lengo la kukuza ustawi wa jamii, mamlaka na hatua hizo za kiutawala zinapaswa kulinda na sio kuzuia utendaji kazi wa Watetezi wa Haki za Binadamu.

**k)**Mashtaka ya jinai na madai yanayofunguliwa na serikali dhidi ya Watetezi (HRDs), kama yale yanayofunguli-

wa dhidi ya watu binafsi na mashirika, yanapaswa kuzingatia misingi ya sheria na usawa mbele ya sheria.

**l)**Serikali haipaswi kuwaingilia Watetezi wa Haki za Binadamu pale ambapo wanafanya kazi na vyombo vya habari vya ndani na nje ya nchi wakati wa uchaguzi na kwenye michakato yote ya kidemokrasia.

**m)**Serikali na Watetezi wa Haki za Binadamu wana wajibu wa kukuza uhuru wa Watetezi (HRDs), utawala binafsi na kanuni za kuwaongoza watetezi nyakati za uchaguzi.

**n)**Watetezi wa Haki za Binadamu wataheshimu haki za msingi za binadamu na uhuru wa utamaduni wa jamii na imani za kidini wakati walikishiriki katika nyakati za uchaguzi.

# KANUNI ZA UTENDAJI

## 2.0 Malengo ya Kanuni

Malengo ya kanuni hizi ni kuweka utaratibu na kanuni za msingi ambazo zitasimamia mwenendo mzima, na kutoa mwongozo wa namna ya utendaji wa watetezi wa haki za binadamu (HRDs) wanapojihusisha na uchaguzi pamoja na michakato ya kidemocrasia. Zitakuwa kanuni rasmi zitakazotumika kuwaongoza watetezi wa haki za binadamu hasa wanachama wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania.

**Kanuni za utendaji zinakusudia;**

**a.** Kutoa uelewa kwa watetezi (HRDs) kuhusu majukumu yao nyakati za uchaguzi

**b.** Kuwaongoza watetezi wa haki za binadamu katika uangalizi na usimamizi wa mchakato wa uchaguzi nchini Tanzania

**c.** Kukuza uelewa juu ya haki pamoja na fursa za watetezi wa haki za binadamu zinazopatikana katika uchaguzi na mchakato mzima wa kidemokrasia

kutoa maarifa kwa watetezi wa haki za binaadamu kuhusu namna ya kushiriki kwa usalama, ufanisi, bila kupendelea upande wowote katika uchaguzi na mchakato wa

kidemokrasia

## 2.1 Wigo wa Kanuni

Kanuni hizi zitatumika Tanzania bara na Zanzibar. Zitatumika kusimamia na kuratibu wanachama waliosajiliwa na ambao hawajasajiliwa pamoja na wanachama muhimu wa Mtandao (THRDC).

### Watetezi (HRDs) Watalazimika Kuzingatia Kanuni Zifuatazo Kipindi cha Uchaguzi

**2.2.1** Watalazimika kuelewa na kuzingatia sheria za ndani pamoja na za Kimataifa za uchaguzi, kanuni na marekebisho yoyote yatakayojitokeza.

**2.2.2** Watatoa elimu ya uraia na ya wapiga kura kwa mujibu wa sheria zilizopo.

**2.2.3** Watashirikiana na Tume za Uchaguzi (NEC, ZEC), Vyombo vya Habari na wadau wengine muhimu katika kutoa elimu ya uraia na ya wapiga kura.

**2.2.4** Watetezi wataandaa ajenda na ilani za uchaguzi kwa umma.

**2.2.5** Watetezi (HRDs) wataendesha mijadala ya umma na majadiliano juu ya masuala yanayohusiana na uchaguzi na demokrasia

**2.2.6** Watetezi watasimamia uchaguzi na kufuatilia mwenendo wa uchaguzi kwa lengo la kujiridhisha kama mchakato huo unakidhi viwango vya kitaifa na kimataifa.

**2.2.7**Watetezi watazingatia na kufichua maovu yatakayojitokeza katika shughuli za uchaguzi na kutoa mapendekezo muhimu.

**2.2.8** Watetezi watakuwa na jukumu muhimu la kuwezesha mchakato wa uchaguzi kuwa huru na wa haki bila ya vurugu na vitisho, kwa kushirikiana na wadau wengine.

**2.2.9** Watetezi watatoa taarifa juu ya vikwazo vyovyote, mashambulizi au vitisho dhidi yao kwa vyombo vya usalama, Mtandao na mashirika mengine yanayohusika.

**2.2.10**Watetezi wanapaswa kuzingatia tamaduni na misingi iliyopo kwenye kanuni hizi.

**2.2.11**Watetezi binafsi au kwa pamoja wanaweza kutafuta rasilimali kwaajili ya kufanya kazi nyakati za uchaguzi na michakato ya Kidemokrasia

**2.2.12**Watetezi hawatajihusisha na shughuli za kisiasa kwa kuunga mkono au kupinga chama chochote cha siasa au mgombea wa ofisi ya umma (ikiwa ni pamoja na kutoa au kupokea fedha au kuhalalisha), wala kutumia rasilimali za watetezi hazitatumika kwa madhumuni hayo.

**2.2.13** Watetezi katika kipindi chote cha uchaguzi, hawatovaaa nguo zenye rangi za kisiasa, beji au kutumia misemo, na hawapaswi kupokea upendeleo wowote wa kisiasa kutoka kwa vyama vya kisiasa au wagombea.

**2.2.4** Mtetezi yeyote wa haki za binadamu haruhusiwi kugombea ofisi yoyote ya kisiasa wakati yeye ni kiongozi au mfanyakazi wa AZAKI

**2.2.15**Ikiwa mwanachama wa Mtandao (THRDC) anatarajia kugombea nafasi ya kisiasa na akishatangaza nia, atalazimika kujiuzulu kutoka nafasi yake mwezi mmoja (1) kabla ya kuanza rasmi kwa kampeni za uchaguzi.

**2.2.16** Ikiwa mwanachama wa THRDC atateuliwa au kuchaguliwa katika ofisi ya kisiasa (ndani ya serikali, bunge au chama cha siasa), atakoma kuwa mwanachama na shirika lake litachagua mtu mwingine kuchukua nafasi yake mara moja

# UTEKELEZAJI NA USIMAMIZI WA KANUNI

## 3.0 Utekelezaji

Kutakuwa na ngazi mbili za utekelezaji wa kanuni hizi za utendaji wa Watetezi (HRDs): Viongozi wa Kanda, (ZCUs) na Sekretarieti ya Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania.

Mtandao kupitia kwa viongozi wa kanda (ZCUs), utaratibu na kusimamia utekelezaji wa kanuni hizi. Mtandao kupitia kwa viongozi wa kanda (ZCUs), utatoa ushauri, mapendekezo kwa wanachama na kwa Watetezi wa Haki za Binadamu au kwa mwanachama muhimu.

Mratibu wa Kitaifa wa Mtandao, inapobidi atatoa onyo la busara kwa mwanachama wa THRDC, ambaye matendo au tabia yake inakiuka kanuni hizi.

Kushindwa kuzingatia onyo hilo, hatua na taratibu zingine za kinidhamu zitachukuliwa kwa mujibu wa Katiba ya Mtandao (THRDC). Uvunjaji wa kanuni hizi ni moja ya makosa ya Kikatiba chini ya Katiba ya Mtandao.

Viongozi wa Kanda (ZCUs), watatoa ripoti mara mbili kwa mwaka juu ya maendeleo ya utekelezaji wa kanuni hizi nyakati za uchaguzi. Dawati la Wanachama THRDC, litawasilisha ripoti ya pamoja ya Viongozi wa Kanda kwa Mratibu wa Kitaifa wa Mtandao.

Kanuni hizi zitabadilishwa mara kwa mara kulingana na mapendekezo ya Watetezi wa Haki za Binadamu (HRDs) na maazimio ya wanachama.

Kanuni hizi zimetolewa kwa mujibu wa Katiba ya Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu, Sera ya Uanachama wa Mtandao na Miongozo ya Viongozi wa Kanda (ZCUs). Uvunjaji wa Kanuni hizi utashughulikiwa kwa mujibu wa nyaraka tajwa hapo juu